

This question paper contains 3 printed pages.

7947

Your Roll No.

Diploma

SWAHILI— Paper I

Time : 3 hours

Maximum Marks : 100

*(Write your Roll No. on the top immediately
on receipt of this question paper.)*

*All questions are to be answered.
All questions carry equal marks.*

Use of dictionary is allowed.

1. Translate the following passage into English:

Usiku ule nikapanda juu ya mti karibu ya hema la yule marehemu nikitumai kwamba wale simba watarudi tena kuja kuchukua mtu mwingine. Kule juu ya mti nalifuatwa na makuli wachache waliokuwa na hofu wakataka niwe nao kule juu; wengine wote waliobaki walijifungia kabisa mahemani mwao. Safari hii hakuna hema lililoachwa mlango wazi. Nalikuwa na bunduki yangu ya mianzi miwili, nami nikawa nimekwisha ishindilia. Baadaye nikasikia sauti ya ngurumo zao zikizidi kunisonga niliko, nikatumai kuwa sasa nitaweza kufanya lo lote. Punde si punde nikasikia kimya kwa kitambo cha saa au mbili hivi, kwani ni tabia yao.

20

2. Translate the following passage into English:

P. T. O.

Katika mkasa huò, watu kadha wa kadha walilala nje kwa sababu ya kutaka upepo, wakifikiri kwamba simba wamekwenda zao kabisa nao hawatarudi tena. Usiku huo simba mmoja alionekana akijipenyeza kutaka kuingia bomani. Mara ikiwa kuvurumisha mawe, magongo, vijinga vya moto upande ule alikopenyea yule simba. Hayo yote simba hayakumzuia kitu, kwani naye alijitoma katikati ya genge la watu akamnyakua mmoja akatoka naye nje katika boma la miiba. Huko nje ya boma akasaidiwa na mwenziwe. 20

3. Translate the following passage into English.

Basi nyani mmoja alikuwa na mtoto wake mdogo, akamwambia, Mwanangu, tunao adui hapa, ndio wanadamu. Watu wakifika shambani kutufukuza, usikimbie peke yako kupanda mtini, au utapatwa, wala usirukeruke ovyo na kwenda mbali nami, au utapatwa tu, ila wosia wangu ndio huu. Nikiwaona watu wanakuja, na wenzetu wengine wanakimbia, sitakimbia mara moja, ila nitasimama tu. Nawe unitazame basi, na ukiona nimesimama pale, unirukie mara moja na kunishika sana. Je, waona manyoya haya ya kifuani mwangu? Basi nishike sana mwa mkono mmoja ushike hapa, na mkono mmoja ushike hapa, na kwa miguu, unishike sana vile vile. 20

4. Translate the following passage into English:

Mwewe akatelemka penye maji, akaenda kunywa. Sungura vile vile akafika pale, akafikiri, Nitamvizia huyu Mwewe, maana yeye ni adui yangu, ndipo

nitampata na Njiwa pia. Akaenda akajilaza kimya-a mdomo wazi, macho yamefungwa, pua inzi wanaingia ovyo. Akafika Mwewe pamoja na Njiwa. Mwewe akamwambia, Sasa nitampata Sungura. Sungura naye akafikiri, Aa, ningoje akinigusa tu nitamshika. Akalala kimya-a. Mwewe akamwambia Njiwa, Wewe je, humli Sungura? Si utamu wa nyama huu! tutakuwa na uhondo leo. Njiwa akanywa hata akashiba, akaondoka r-r-r!

20

5. Do you agree that the composition of stories in 'Hadithi za Kiabrika zimekuwa za kikristo' lays emphasis on morals of a good man.

Or

Why was the project of building a rail line disrupted and delayed through the National Park of Tsavo in East Africa?

20